# JIMBO KATOLIKI LA RULENGE – NGARA

# ST. CLARE BIHARAMULO GIRLS' SECONDARY SCHOOL


**P.O BOX 34, BIHARAMULO – KAGERA** **+255755 797 006**

info@stclarebiharamulo.ac.tz www.stclarebiharamulo.ac.tz


# JOINING INSTRUCTIONS FORM

## (FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2027)

**KWA MZAZI WA** ______________________________________________

**PAROKIA YA** ____________________________ **JIMBO LA** __________________________




***Motto:*** *Education for Serving with Integrity*
*(Elimu kwa ajili ya kutumikia kwa Uadilifu)*

***Vision:*** *A highly motivated, well disciplined and excellent performing School*
*(Shule yenye Hamasa, Nidhamu nzuri na inayofanya vizuri sana)*

P.O Box 34, Biharamulo – Kagera +255755797006 info@stclarebiharamulo.ac.tz www.stclarebiharamulo.ac.tz

## FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2027

Ndugu: ______________________________________________________________________________

**YAH: <u>KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA 2025.</u>**

Ninafurahi kukufahamisha kuwa umechaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari ya Wasichana St. Clare Biharamulo. Shule hii ni kituo cha malezi ambapo vijana hulelewa katika maadili ya Kikatoliki. Pia wanafunzi hufundishwa masomo ya kawaida ya sekondari. Sala, mafungo ya mara kwa mara na maelekezo ya kiroho husisitizwa. Maisha ya **uadilifu, uaminifu, utii, nidhamu na unyenyekevu** hutiliwa mkazo ili kuleta ufanisi katika kazi zote.

Unatakiwa kufika shuleni St. Clare Biharamulo siku ya **Jumatatu** tarehe **11/01/2027.** Ninakupatia fomu ya tamko ambayo unatakiwa kuijaza na kuirejesha shuleni wakati unapokuja.

**MAHALI SHULE ILIPO:** Shule ya Sekondari ya Wasichana ya St. Clare Biharamulo inapatikana kata ya **Biharamulo Mjini** katika eneo liitwalo **Rukaragata** kilometa 2.5 kutoka stendi ya mabasi ya wilaya ya **Biharamulo** mkoani **Kagera**.

**USAFIRI:** Mzazi / Mlezi atamsafirisha mwanae kutoka nyumbani hadi shuleni ambapo atamkuta mwalimu wa zamu atakayempokea na kumpa maelekezo muhimu.

**RATIBA YA MAPOKEZI:** Mwanafunzi atapokelewa siku za Jumatatu hadi Jumamosi kuanzia saa 2:00 asubuhi (saa mbili kamili asubuhi) hadi saa 12:00 jioni (saa kumi na mbili kamili jioni). **Siku ya Jumapili hakuna mapokezi.**

## MAHITAJI YA SHULE

1. **CHETI CHA KUZALIWA**: Mwanafunzi anatakiwa kuja na nakala (copy) ya cheti cha kuzaliwa. Asiyekuja na cheti hicho hatapokelewa.

2. **ADA / KARO:** Ada ya masomo ni shilingi **Milioni moja na laki nane (Tshs. 1,800,000/=)** kwa mwaka ambayo inaweza kulipwa mara moja au kwa awamu nne kama ifuatavyo;
   (i). January (Mwezi wa kwanza) – 450,000/=
   (ii). April (Mwezi wa nne) – 450,000/=
   (iii). July (Mwezi wa saba) – 450,000/=
   (iv). September (Mwezi wa tisa) – 450,000/=

   **ZINGATIA**: Malipo yote yafanyike kupitia **Benki ya NMB Akaunti namba 31706600246**, Jina la Akaunti ni **ST.CLARE GIRLS SECONDARY SCHOOL** na mlipaji asisahau kuandika **Jina la Mwanafunzi** anayelipiwa ada hiyo kwenye hati ya malipo**.**

3. **SARE ZA SHULE:** Sare za darasani (2), Sketi za kijani (2), Tisheti (2), Sweta, Sare za michezo, Sare ya kazi za nje, Passport size, Kitambulisho cha shule, Kitabu cha mwongozo wa misa ya kingereza (The order of Mass) na Vyombo vya kulia chakula. Vitu vyote hivyo atavipata shuleni kwa malipo ya shilingi **Laki tatu na Elfu sitini (Tshs. 360,000/=).** Pesa hii ilipwe kupitia Benki ya **NMB Akaunti namba 31706600246 (ST. CLARE GIRLS SECONDARY SCHOOL).**

4. **BIMA YA AFYA:** Mpendwa Mzazi / Mlezi unakumbushwa kumpatia mwanao Bima ya Afya aje nayo shuleni. Kama hana, unatakiwa kumlipia shilingi **Elfu hamsini na Mia nne (Tshs. 50,400)** kwa ajili ya kumkatia Bima ya Afya ya NHIF hapa shuleni. **<u>HITAJI LA BIMA YA AFYA NI LA LAZIMA KWA KILA MWANAFUNZI</u>**. Pesa hii iletwe mkononi wakati wa kuripoti shuleni (**ISILIPWE** kupitia Benki)

5. **VIFAA VYA DARASANI:** Mwanafunzi anatakiwa kuja shuleni akiwa na vifaa vifuatavyo;
   (i). Dictionary (English – English) – 1
   (ii). Kamusi ya Kiswahili sanifu toleo la 04 – 1
   (iii). Dictionary ya Kifaransa – 1
   (iv). Biblia ya Kingereza – 1
   (v). Daftari kubwa (Counter books Quire 2) – 15
   (vi). Daftari za Msomi au Master – 13
   (vii). Spring plastic file – 1
   (viii). Box file kubwa – 1
   (ix). Mathematical Set (Oxford) – 1
   (x). School bag – 1
   (xi). Kalamu za wino – 10
   (xii). Penseli na mifutio – 5
   (xiii). Rula nzito (Revlon) – 2
   (xiv). Ream (Double A) – 2(Kwa mwaka)

6. **VIFAA VYA BWENINI:** Mwanafunzi anatakiwa kuja shuleni akiwa na vitu vifuatavyo;
   Godoro la futi 2 ½ , Blanketi nzito 1, Solata 1 (siyo tochi),Viatu vya masai visivyo na urembo wowote, Viatu vyeusi vya kamba vyenye visigino vifupi – Pair 2, Raba nyeupe – Pair 1, Tracksuit ya kijani – Pair 1, Shuka 3 za rangi ya Pink Jinja, Mwamvuli mmoja wa size ya kati, Soksi nyeupe ndefu (Stocking) – Pair 3, Beseni la Plastic – 1, Ndoo moja ya plastiki ya lita 20, Dawa ya viatu vyeusi (kiwi), Brush ya viatu, Chandarua cha bluu pamoja na sanduku la chuma au la mbao kwa ajili ya kuhifadhia vitu vyake.

7. **MAHITAJI BINAFSI YA MTOTO WA KIKE:** Mtoto wa kike anatakiwa kuwa na yafuatayo;
   Chupi – 5 au zaidi, Taiti – 5 au zaidi, Under skirt – 2, Kanga ya kuogea – 1, Uzi na sindano, Pedi, Magazeti ya kuhifadhia pedi iliyotumika – Kg1, Ndala za kuogea, Toilet paper – 6, Sabuni – Miche miwili, Kitana na Mafuta ya kujipaka yasiyo na kemikali

   **KUMBUKA:** Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na vipodozi vya aina yoyote ikiwa ni pamoja na losheni (lotion), sabuni zenye kemikali na manukato (perfume).

   Pia ikumbukwe kuwa mwanafunzi afikapo shuleni hatakuta sare ya shule ikiwa tayari imeshonwa. Hivyo basi, anatakiwa aje na nguo za heshima jozi (pair) 4 ambazo atazitumia kwa muda mfupi na kuzirudisha nyumbani wakati wa likizo fupi.

8. **VIFAA VYA USAFI:** Mwanafunzi anatakiwa kuja na vifaa vifuatavyo;
   - Mfagio laini wa ndani (Soft broom) – 1
   - Mpira wa kuvutia maji (Squeezer) – 1
   - Mfagio wa nje (Chelewa) – 1
   - Jembe na mpini wake – 1

## TAARIFA NYINGINE

1. **CHAKULA:** Chakula kikuu hapa shuleni ni ugali na Maharage pamoja na uji kwa kifungua kinywa. Mzazi anayejua kwamba mtoto wake hatumii vyakula hivi basi tunamsihi asipokee nafasi hii.
   **NB**: Vyakula vingine kama nyama, wali, mboga za majani pamoja na matunda hutolewa kulingana na utaratibu.

2. **UZALISHAJI MALI:** Kila mwanafunzi anatakiwa kushiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji kwa lengo la kuhitaji kumjenga katika stadi za kazi na za maisha.

**“URITHI WA MTOTO NI KUPATA ELIMU BORA”**
**TUNAMTAKIA SAFARI NJEMA YA KUJA SHULENI ST. CLARE BIHARAMULO**
**KARIBU SANA**

Kwa maelezo na mawasiliano zaidi, tupigie simu kwa namba zifuatazo;

| | | | |
|---|---|---|---|
| **0755-797-006** (Mkuu wa Shule) | **0765-281-363** (Makamu Mkuu wa Shule) | **0768-944-226** (Mtaaluma Mkuu) | **0757-651-708** (Mtaaluma Msaidizi) |

# SHERIA ZA SHULE

Kila Mwanafunzi wa St. Clare Biharamulo anapaswa azingatie yafuatayo;

1. **HESHIMA.**
   - Mwanafunzi asimame na kumsalimu Mwalimu au mtu yeyote anayemzidi umri anapopita, aingiapo darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.
   - Mwanafunzi asitumie lugha mbaya kati yake na mwenziye, kati yake na Mwalimu / Mfanyakazi au mtu yeyote.
   - Kila mwanafunzi awaheshimu wafanyakazi wote waliopo Shuleni.
   - Kila mwanafunzi athamini na aheshimu kila aina ya kazi shuleni. Pia kila mwanafunzi ashirikiane na kusaidiana kazi kati yake na mwanafunzi mwenziye.
   - Mwanafunzi haruhusiwi kufuga kucha, kuwa na nywele ndefu, kuvaa mavazi yasiyo ya heshima, au urembo wa aina yoyote ambao unaweza ukapotosha lengo la mwanafunzi kama vile mavazi ya kubana, mikufu, lip – shiner, lip – bum, kupaka hina, perfume au mafuta ya manukato ya aina yoyote. **Vyote hivi haviruhusiwi.**
   - Kila mwanafunzi aitikie wito wa kengele au wito wowote mara moja.
   - Kila mwanafunzi azingatie kanuni za Kikatoliki awapo Kanisani.
   - Kila mwanafunzi hana budi kuheshimu Bendera ya Taifa, Serikali, Nembo ya Taifa (Court of arms), Wimbo wa Taifa na Fedha za Taifa.
   - Kila mwanafunzi aheshimu Ukumbi wa mikutano, Bwalo la chakula, Ofisi za walimu, Ofisi ya Mkuu wa Shule, Mali ya umma na Mali binafsi.
   - Kila mwanafunzi akae kimya wakati wote darasani, aombe ruhusa wakati wa kutoka nje, na anyooshe mkono na asimame wakati wa kuuliza au kujibu maswali. Kila mwanafunzi awe mfano bora wa heshima na tabia njema mahali popote ndani na nje ya shule.

2. **KUSALI**
   - Kila mwanafunzi lazima awepo na ashiriki Misa na sala zote zinazosaliwa shuleni kadri ya utaratibu.
   - Baada ya sala za 4:00 usiku, kila mwanafunzi awe kimya (Complete Silencium / Absolute Silence), aelekee bwenini akiwa kimya. Atakayekaidi atachukuliwa hatua za kinidhamu.

3. **MAHUDHURIO.**

(i). Kila mwanafunzi hana budi kuhudhuria vipindi muda wote wa masomo.

**Muhimu:**

- Kila mwanafunzi atakayeshindwa kufikisha wastani wa shule wa alama 50% atashauriwa kutafuta shule nyingine.
- Lugha kuu za mawasiliano wakati wote ni Kiingereza na Kifaransa.
- Kazi za mikono ni lazima kwa wote.

(ii). Kila mwanafunzi ni lazima kuhudhuria mikutano ya shule, kwa mfano Baraza la shule, Ukaguzi wa Usafi, Mikutano / vikao vya mabwenini na madarasani, kupandisha bendera ya Taifa, Paredi n.k.

4. **KUWAHI.**
   - Kila mwanafunzi ni lazima kuwahi shughuli zote za shule kama zilivyopangwa katika ratiba ya kila siku.
   - Wakati wa kufungua shule, kila mwanafunzi ni lazima afike shuleni tarehe zilizopangwa. Atakayechelewa siku iliyotajwa aletwe na mzazi, mzazi ataeleza sababu za kuchelewa kwa mwanae.
   - Itokeapo dharula yoyote kila mwanafunzi afike mara moja mahali husika asikiapo wito wa kengele.
   - Majina yataitwa (Roll Call) kila mara, atakayekosekana wakati huu atakuwa amejifukuza shule.

5. **SARE ZA SHULE.**
   - Sare za shule ni lazima zivaliwe wakati wa masomo darasani, kutoka nje ya shule kwa shughuli za shule, mhadhara wa shule (School baraza), kwenda hospitali. Wanafunzi watakapokuja shuleni au kwenda makwao nyakati za likizo pia kuvaa sare za shule ni lazima.
   - Wakati wa michezo kila mwanafunzi avae mavazi ya michezo aliyoelekezwa.
   - Kofia, viatu vyenye visingino virefu na mapambo ya aina yoyote **haviruhusiwi shuleni.**
   - Sare na mavazi yote ni lazima yawe safi siku zote na yawekewe alama.

6. **MIPAKA YA SHULE.**
   - Mwanafunzi asitoke nje ya mipaka ya shule isipokuwa kwa kibali maalumu cha maandishi na muhuri kutoka kwa Mkuu wa Shule.
   - Wanafunzi hawaruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalum. Chumba cha Walimu (Staff Room), Ofisi za shule, Maabara, Jiko na Stoo ya Chakula, Nyumba za walimu na za wafanyakazi wasio walimu.
   - Uongozi wa shule utatoa ruhusa ya kwenda maeneo yaliyotajwa hapo juu pale inapofaa kufanya hivyo.

7. **WAGENI.**
   - Mwanafunzi ataruhusiwa kuonana na wageni wake kwa ruhusa maalumu kutoka kwa Mkuu wa Shule.
   - Wazazi wa wanafunzi watafika kujua maendeleo ya watoto wao siku za kawaida za juma kutoka kwa walimu wa madarasa au ofisi ya Mkuu wa shule kwa utaratibu utakaoelekezwa na Mkuu wa shule kila mwaka.
   - Mgeni wa mwanafunzi atapokelewa kwa heshima na adabu.
   - Wanafunzi wawasalimie wageni wote wafikao shuleni.

8. **MAKOSA: Makosa yatakayosababisha kujifukuza shuleni mara moja ni pamoja na**;
   - Wizi, uongo, ukaidi na utoro (wizi wa vifaa na matunda)
   - Uasherati, kutoa mimba, kuolewa, matumizi ya vifaa vya kuzuia mimba
   - Uvutaji wa Bangi na matumizi ya madawa ya kulevya
   - Makosa ya jinai (mfano kutaka kujiua)
   - Kupigana, matumizi ya lugha chafu
   - Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
   - Ulevi wa aina yoyote
   - Kuwadharau walimu na walezi.
   - Kudharau Bendera ya Taifa
   - Kupata mimba
   - Kukosa kusali
   - Kushiriki katika migomo na maandamano
   - Kumiliki simu, redio au vifaa vya umeme **(Haviruhusiwi shuleni)**
   - Ni marufuku kuja na chakula aina yoyote shuleni
   - Kukutwa kitandani wamelala zaidi ya mwanafunzi mmoja
   - Kutumia mafuta / vipodozi vyenye kemikali (vya kuchubua)
   - Kosa ambalo kwa uzito wake linastahili adhabu ya aina hii

9. **UGONJWA.**
   - Ugonjwa wa aina yoyote lazima uelezwe wazi mapema kwa mtaalamu wetu wa afya au kwa Mkuu wa shule pindi mwanafunzi anaporipoti shuleni.
   - Ni marufuku kutumia dawa za kienyeji kwa siri. Dawa zote lazima zioneshwe kwa Nesi au kwa Mkuu wa Shule. Ukigundulika kuwa na dawa za kienyeji kinyume cha utaratibu utajifukuza shule.
   - Mwanafunzi yeyote asilale bwenini bila taarifa na ruhusa ya Nesi na pia ruhusa hiyo ni vyema Mwalimu wa zamu akafahamu ili kujua idadi ya wagonjwa waliolala dispensary / sick bay na waliolazwa hospitalini ili awaorodheshe kwenye daftari la taarifa la zamu.

10. **SIMU NA BARUA.**
   - Ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na simu shuleni.
   - Barua zote za wanafunzi zinazotoka na kuingia lazima zipitie Ofisi ya Mkuu wa Shule.
   - Mwanafunzi atapata nafasi ya kuwasiliana na Mzazi / Mlezi wake kupitia kwa Mfanyakazi aliyepewa jukumu hilo.

11. **USAFI NA UHIFADHI WA MAZINGIRA.**
   - Kila mwanafunzi sharti ahakikishe maeneo yanayomzunguka ni safi. Hii ni pamoja na kupamba mazingira ya shule kwa kupanda na kumwagilia maua, miti na bustani za matunda na mboga mboga.
   - Usafi wa vyumba vya madarasa na mabweni ni lazima uzingatiwe. Atakayekaidi kufanya usafi atajichukuliwa hatua za kinidhamu.

**KILA KITU KINAWEZEKANA KWA MUNGU**
**Rev. Dr. Dagobert Kabendera (PhD)**
**Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Wasichana St. Clare Biharamulo.**

**TAMKO LA MZAZI / MLEZI WA MTOTO ALIYECHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA YA ST. CLARE BIHARAMULO YA JIMBO KATOLIKI LA RULENGE – NGARA.**

Katika kipengele cha 1, 2 na 3 kata neno lisilo chaguo lako kati ya haya yaliyoko kwenye mabano.

1. Binti yako amechaguliwa kujiunga na shule hii:
   - Je, Mzazi uko tayari kumsaidia mtoto wako kwa kumlea vizuri ili baadaye awe raia / muumini mzuri, muadilifu, mnyenyekevu? (Ndiyo / Hapana)
2. Binti atakayekuwa na tabia mbaya shuleni lazima aondolewe na kutafutiwa shule nyingine kwani kuna makosa ambayo hayavumiliki shuleni.
   - Mzazi utakuwa tayari kumtafutia shule nyingine mwanao atakapoonekana hazingatii maadili ya shule na ya Kanisa? (Ndiyo / Hapana)
3. Shule hii haipati ruzuku kutoka Serikalini wala mahali popote, ila inaendeshwa kwa karo na michango ambayo inatolewa na mzazi wa mwanafunzi.
   - Kwa sababu karo inaweza kupanda, utakubali kulipa karo kiasi kitakachopangwa na Bodi ya shule wakati mwanao yupo shuleni? (Ndiyo / Hapana)
4. Mwanao ana ugonjwa au tatizo la kudumu? Eleza wazi (usipoeleza mwanao akigundulika baadaye kuwa mzazi hukuwa mkweli mwanao atarudishwa nyumbani mara moja). Fahamu kuwa shuleni wanafunzi wote ni sawa hakuna chakula maalumu au “Special diet”. Ugonjwa wa mwanangu ni ____________________________________
   ______________________________________________________________________________________________
5. Iwapo kuna haja ya mawasiliano ya dharula toa orodha ya wanaoweza kuelezwa.

| Na | Jina | Anapoishi (Wilaya) | Uhusiano | Namba ya simu |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | Baba / Mlezi | |
| 2 | | | Mama / Mlezi | |
| 3 | | | | |
| 4 | | | | |

6. Mimi ___________________________________ (Baba) na __________________________________ (Mama) / Mlezi tunatoa tamko kuwa **TUTALIPA MALIPO TULIYOELEKEZWA** kwenye fomu ya kujiunga **BILA MALALAMIKO NA HATUTADAI KUREJESHEWA FEDHA YOYOTE** tukishailipa hata kama mtoto wetu itabidi aondoke shuleni akikiuka maadili. Hakikisha kuwa unapata RIPOTI ya maendeleo ya Taaluma na nidhamu kutoka kwa mwanao kila ajapo nyumbani wakati wa likizo ndefu (Mwezi Juni (6) na Desemba (12)). **Mzazi** hakikisha unasoma vema ripoti ya mwanao na kutoa mrejesho shuleni pale unapolazimika kufanya hivyo.

Majina ya Baba __________________________________________ Saini __________________ Tarehe: _________________

Majina ya Mama _________________________________________ Saini __________________ Tarehe: _________________

**Iwapo mtoto analelewa na ndugu tofauti na wazazi**

Jina la Mlezi: _________________________________ Uhusiano: ________________ Saini __________ Tarehe: __________

**TAMKO LA MWANAFUNZI**

Mimi _____________________________________________ ninakubaliana / sikubaliani na maelekezo na sheria nilizopewa. Nitatenda **HAKI,** ninaleta **AMANI,** nitakuwa **MTIIFU, MWADILIFU, MNYENYEKEVU, MKWELI, MWAMINIFU** na **NITAWAHESHIMU** wakubwa na wenzangu wote. Nitaliheshimu **TAIFA** na **KANISA KATOLIKI** na wahudumu wake wote niwapo shuleni na ninapokuwa nje ya shule. Nitajitahidi kitaaluma kuvuka wastani wa shule ambao ni 50% kwa sasa na iwapo sitafikisha wastani wa shule nitakubaliana na hatua zitakazochukuliwa dhidi yangu.

Jina la mwanafunzi __________________________________________ Shule ya Msingi aliyotoka: ______________________

Namba ya Mtihani: ________________________________ Sahihi: ____________________ Tarehe: ____________________

**KUMBUKA: LENGO LA SHULE** ni kutayarisha raia bora wa kesho, kwahiyo mtoto wako anatakiwa awe na Moyo wa IBADA, HESHIMA NA NIDHAMU. Awe msikivu na mchapa kazi wa darasani na nje pasipo kusukumwa.

Fomu hii irudishwe shuleni siku Mwanafunzi anaporipoti

**Rev. Dr. Dagobert Kabendera (PhD)**
**Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Wasichana St. Clare Biharamulo.**

# MEDICAL EXAMINATION FORM

**Student's Name:** ___________________________________________________________________________

(To be completed by a government Medical Officer)
The examination should include the following categories:

1. B/P: ______________________________________________________________________
2. HB: ______________________________________________________________________
3. BLOOD GROUP: ______________________________________________________________
4. S/CELL: ____________________________________________________________________
5. CHEST: ____________________________________________________________________
6. ASTHMA: ___________________________________________________________________
7. TUBERCLOSIS: _______________________________________________________________
8. HEART DISEASES: ____________________________________________________________
9. EYE SIGHT: ________________________________________________________________
10. HEARING: _________________________________________________________________
11. SPEECH: __________________________________________________________________
12. EPILEPSY: _________________________________________________________________
13. NEUROSIS / PYSCHOSIS: _____________________________________________________
14. ALLERGIES: ________________________________________________________________
15. URINE ANALYSIS: ____________________________________________________________
16. PREGNANCY (UPT): __________________________________________________________
17. PEPTIC ULCER: ______________________________________________________________

**Medical Officer's name:** _______________________________________ **Designation:** ____________________

**Station:** _______________________________________ **Signature:** ______________________

**Date:** ________________________ **Stamp:** _________________________